THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL

CERTIFICATE OF SECONDARY EDUCATION EXAMINATION, 1993

DAREDA SECONDARY SCHOOL
P.O.BOX 344
BABATI

021/1

KISWAHILI - PAPER 1

(Kwa watahiniwa walioko na wasiokuwa shuleni)

MUDA: Saa 3:00

MAAGIZO KWA MTAHINIWA

1. Jibu maswali manane (8) tu, maswali MANNE kutoka sehemu A, na maswali YOTE ya sehemu B.
2. Zingatia maagizo ya kila sehemu na ya kila swali.
3. Kumbuka kuandika namba YAKO ya mtihani katika kila ukurasa wa kijitabu cha kujibia.

Karatasi hii ina kurasa 5 zenye maandishi.

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

Scanned with CamScanner

## SEHEMU A - FASIHI

### KIFUNGU (I) - Fasihi Simulizi

(Jibu swali la 1 AU la 2)

1. (a) Eleza tofauti za hadhira ya Fasihi Simulizi na hadhira ya Fasihi Andishi.
   (b) Kwa nini wakati mwingine Fasihi Simulizi hutumia wahusika wasiokuwa wanadamu?

2. "Fasihi Simulizi ikihifadhiwa katika maandishi hupunguziwa uhai wake kwa kiasi kikubwa." Jadili.

### FASIHI ANDISHI

### KIFUNGU (II) - Ushairi

3. "Wakati hudhibiti usanii wa mshairi". Kwa kutumia vitabu viwili kati ya TEUZI ZA NAFSI, MASHAIRI YA SAADANI na MASHAIRI YA CHEKACHEKA, jadili kauli hii.

AU

4. Ushairi ni silaha madhubuti inayomwonyesha mshairi kuwa mzalendo na shujaa. Kwa kutumia vitabu viwili kati ya TEUZI ZA NAFSI, MASHAIRI YA SAADANI na MASHAIRI YA CHEKACHEKA, dhihirisha kauli hii.

### KIFUNGU (III) Riwaya/Hadithi

5. Kwa kutumia vitabu viwili kati ya SHIDA, KULI na DUKA LA KAYA, jadili watunzi wa riwaya hizo wanavyochangia ujenzi wa jamii mpya.

AU

6. Kati ya SHIDA, KULI na DUKA LA KAYA chagua wahusika wakuu wanaume wawili (mmoja kila kitabu) na uonyeshe jinsi wahusika hao wanavyohamasishwa na wahusika wanawake kutekeleza matendo makuu wayatendayo (hao wahusika wawili).

### KIFUNGU IV Tamthiliya

7. "Uwajibikaji wakati wa kazi ni suala la lazima, na kinyume chake ni maafa kwa mhusika na jamii nzima." Tumia vitabu viwili kati ya HARAKATI ZA UKOMBOZI, HAWALA YA FEDHA na NGOSWE PENZI KITOVU CHA UZEMBE, ujadili kauli hii.

AU

8. "Lugha na matendo ni vigezo muhimu katika kupima kufanikiwa kwa tamthiliya" Kwa kutumia tamthiliya mbili kati ya HARAKATI ZA UKOMBOZI, HAWALA YA FEDHA, na NGOSWE - PENZI KITOVU CHA UZEMBE, thibitisha ukweli wa usemi huu.

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

Scanned with CamScanner

## SEHEMU B: LUGHA

9. UFAHAMU:

Soma kifungu cha habari kifuatacho kisha jibu maswali:

Ukiwauliza baadhi ya watu wa Afrika ya Mashariki: Mswahili ni nani, utapata majibu anuwai: wengi watakujibu ni Mwafrika, wengine watakuambia ni M-bantu, na bado wengine watasema ni mtu mweusi. Alimradi kila mmoja na fikra zake. Na kwa baadhi ya watu Mwafrika ni mtu yeyote aliyezaliwa katika bara la Afrika. Kwa mujibu wa watu hao, Wazungu, Wahindi, Waarabu n.k. waishio sehemu mbalimbali za bara hili nao ni Waafrika pia. Kwa wengine, Waafrika ni watu weusi. Ukweli wa yote haya uko wapi?

Uswahili hii leo si kabila, bali ni mila za watu fulani - pamoja na utumiaji wa lugha ya Kiswahili kuwa lugha iliyowalea na kuwakuza. Uswahili niuzungumziao unatokana na watu waishio Pwani ya Afrika ya Mashariki. Njia bora zaidi ya kuuelewa "Uswahili" ni kuishi huko pamoja na watu hao. Tukifanya hivyo tutaelewa pia ni watu gani wengine ambao hawakuzaliwa Pwani ya Afrika ya Mashariki ambao pia nao ni Waswahili. Nimesema Uswahili si kabila. Lakini hapana Mswahili asiyekuwa na kabila. Kuna Waswahili wenye makabila ya Kiyao, Kitumbatu, Kigunya, Kizigua n.k. Kwa hiyo mtu anaweza kuwa Mswahili na huku akawa Mhindi, Mwarabu, Bulushi, Mzungu, n.k.

Asili ya neno lenyewe Kiswahili ni neno "Sahil", neno linalotokana na lugha ya Kiarabu. Na maana yake kwa lugha hiyo ni pwani. Waarabu hawakulitumia neno hilo kukusudia pwani maalum, bali pwani kwa jumla. Wabantu wenyewe ndio waliolitohoa neno hilo na kuwa "Kiswahili" kusadifu mazingira ya matamshi yao. Hapo awali Waswahili walikuwa watu maalum. Lakini baada ya karne nyingi, mengi yametokea. Ilivyokuwa Uswahili si kabila bali ni utamaduni, desturi na mila za watu fulani waitumiao lugha hii kuwa lugha yao ya maisha, basi yeyote mwenye kutumia lugha hii kwa misingi hiyo ni Mswahili. Vivyo hivyo Uafrika si rangi bali ni ile hali ya mtu kuwa na mizizi yake kwenye bara hili na yeye mwenyewe kuifahamu na kuitumia lugha mojawapo ya wenyeji wa pahala aishipo katika bara hili. Aidha awe mmoja wao kwa mila na desturi zao, na awe na hisia zinazofungamana na bara hili na watu wake.

Tunawashukuru wageni hasa Wazungu, kwa kutuandikia na kutufundisha historia - hata ile yetu wenyewe. Kwa mujibu wa historia hiyo tumesomeshwa kwamba Waarabu ni watu waliopenda kufanya biashara ya watumwa; kwamba Waswahili ndio wachuuzi wa Waafrika wenzao. Imediriki kuandika historia hiyo kuwa Mswahili ni mtu mwenye damu ya mchanganyiko baina ya Waafrika na Waarabu - wafanya biashara ya uovu usiomithilika. Bila shaka - chuki ni stahili yao. Bila shaka

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

Scanned with CamScanner

hata lugha yao Kiswahili, ni lugha ya maovu ya daraja hiyo. Wewe unasemaje?

Ni dhahiri, biashara ya utumwa ni uovu mkubwa kwa ubinadamu. Lakini ujinga pia ni uovu. Kukubali tusomeshwayo shuleni bila kuhoji tusomeshwayo nao ni ujinga. Hivyo, kuikubali historia inayowataja Waswahili na Waarabu peke yao kuwa ndio waliohusika na biashara ya utumwa katika Afrika ni kutaja nusu tu ya ukweli. Walikuweko Waafrika wenzetu walioishi bara ambao waliwahujumu Waafrika wenzetu. Aidha, huko pwani ya Afrika ya Magharibi, Wazungu wa mataifa mengi walifanya biashara ya utumwa, na pengine kwa ukatili zaidi. Ushahidi wa hayo uko katika Wanegro kudai haki zao za kijamii hadi hivi leo. Je, hawa nao walichuuzwa na Waswahili?

Iwapo hatuafiki madai kwamba historia ya Afrika ya Mashariki ilianza pale David Livingstone alipofika pande hizi za Afrika - kama alivyoandika Coupland yatubidi tuiangalie upya historia yetu kwa fikra za kuhoji na kwa kutumia mizani yetu ya adili. Tusipofanya hivyo, hatutakuwa wajinga tena, bali wapumbavu.

MASWALI:

(a) Kwa mujibu wa habari hii, Mswahili hapo awali ni nani?

(b) Mwandishi anasema hivi leo Mswahili ni nani?

(c) Ukweli kamili juu ya wafanyabiashara ya utumwa ni upi?

(d) Kwa nini mwandishi anataka tujifunze upya historia yetu?

(e) Kujifunza kwa kuhoji ni kujifunza vipi?

(f) Fupisha aya ya tatu kwa maneno hamsini au pungufu.

(g) Eleza maana ya maneno yaliyopigiwa mstari.

(i) anuwai

(ii) walioitohoa

(iii) waliwahujumu.

(iv) usiomithilika

10. Andika insha yenye maneno yasiyozidi 250 kuhusu moja ya mada hizi.

(a) Mipango yangu ya baadaye kama sitachaguliwa kidato cha tano.

(b) Upigaji marufuku uvutaji sigara kwenye vyombo vya usafiri

(c) Umuhimu wa kujifunza lugha

(d) ujirani mwema.

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

Scanned with CamScanner

11. (a) Andika E kwa Kielezi au V kwa Kivumishi kwa maneno yaliyopigiwa mstari katika sentensi zifuatazo:

(i) Hata ndege hukaa wawili wawili.

(ii) Viti hivi vizuri .

(iii) Mariam anaimba vizuri.

(iv) Macho yake malegevu.

(v) Kitanda cha kwanza kushoto ndicho alicholalia.

(b) Eleza kazi za mofimu u katika sentensi zifuatazo:

(i) Utaratibu huu ni mzuri

(ii) Ujumbe unaoufuata ni wa siri.

(iii) Wewe u mtoto wa kaka yangu.

(iv) Ungelijua usingesubiri.

12. Changanua sentensi hizi kwa kutumia njia ya jedwali

(a) Usipowasikiliza wazazi wako mwanangu utaharibikiwa.

(b) Musa anajigamba sana lakini sisi tumemdharau.

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

Scanned with CamScanner